

23:1-24:33 YOSHUA ANAAGA

Hatuna habari kuhusu mambo yaliyotokea kati ya kazi ya Yoshua ya kugawanya nchi na hotuba yake ya mwisho kwa taifa lake miaka mingi baadaye. Wakati huo, Yoshua akiwa mzee sana (taz.mst.14), naye aliwaita viongozi wa Israeli ili awape mausia ya faraja na maonyo (23:1 -2). Aliwahakikishia kwamba Mungu angeendelea kuwapigia vita mpaka Wakanaani wote waliobaki wafutiliwe mbali, mradi tu wao wawe waaminifu kwa agano. Mambo muhimu zaidi yangukuwa kumpenda BWANA Mungu wao, watimize sheria zake na wajiepushe na ibada ya miungu mingine (3-11). Aliwaonya wasioane na watu wa mataifa yaliyokuwa kati yao (12-13), nao wakumbuke kwamba uaminifu kwa Mungu ungewaletea baraka ya daima, lakini uasi ungewaletea hukumu (14-16).

Kama vile Waisraeli walivyokuwa wamethibitisha agano huko Shekemu kabla ya kuiteka nchi (8:30-35), hata wakati huo viongozi kwa niaba ya watu walikutana tena huko wakathibitisha upya uaminifu wao kwa agano (24:1). Chanzo cha agano kilikuwa kwa Mungu aliyekuwa amemleta Ibrahimu kutoka Mesopotamia akamwingiza Kanaani na kumwahidi kuwafanya wazao wake kuwa taifa kubwa na kuwapa Kanaani kuwa nchi yao wenyewe (2-4). Baada ya karne kadhaa Mungu alitimiza ahadi hiyo alipowaleta Waisraeli kutoka Misri (5-7), kupitia jangwa la Sinai (8-10) na mwisho kuwaingiza Kanaani (11-13). Lakini Waisraeli walikuwa wameonyesha mvuto wa kupenda ibada ya miungu, ikiwa ni ibada ya miungu ya wazazi wa Ibrahimu, au ya Wamisri, au ya Wakanaani ambao waliteka nchi yao. Kwa sababu hiyo walipaswa kufanya uamuzi maalumu, ama kumwabudu mmojawapo wa miungu ile, au kumwabudu BWANA (YAHWEH) (14-15).

Tena kwa upesi sana watu waliahidi kumtumikia BWANA peke yake (16-18). Yoshua alijua kwamba kuahidi uaminifu kulikuwa rahisi, lakini kuutumiza siyo rahisi namna hiyo. Kwa hiyo aliwaonya watu tena juu ya matokeo ya hatari kubwa, kama wangevunja agano la Mungu Mtakatifu namna hii (19-20). Watu walipoapa kwamba walijua walichokiamua, Yoshua aliwataka wathibitishie ahadi yao ya uaminifu pale pale (21-24). Kisha katika sherehe maalumu alitia muhuri agano, akaandika tena sheria zote ambazo watu walipaswa kuzitimiza, akasimamisha jiwe kubwa kuwa ushahidi wa ahadi ya watu ya kutimiza agano (25-28).

Yoshua alikufa akijua kwamba uongozi wake ya Yusufu, na hivyo ilitimizwa imani ya thabiti uliwasaidia watu washike uaminifu wao matumaini yake ya karne nyingi zilizopita, kwa Mungu. Alizikwa katika eneo la nchi yake alipoonyesha imani katika ahadi za Mungu mwenyewe iliyokuwa katika eneo la kabila lake la (32; Mwa 50:24-25; Kut 13:19; Ebr 11:22). Efraimu (29-31). Maiti ya Yusufu iliyoletwa Kuhani mkuu pia alizikwa katika eneo la Efraimu kutoka Misri, pia ilizikwa katika eneo la makabila (33).